Kinamilikiwa na:

(andika jina lako hapa)

EU UNIVERSE AWARENESS

# ULIMWENGU Mfukoni Mwako Kitabu cha Mazoezi Kimeandaliwa na

**ULIMWENGU** ni jumla ya kila kitu ambacho kipo: kama sayari, nyota, galaxi pamoja na vitu vingine vyote vipatikanavyo angani.

**GALAXI** ni mkusanyiko mkubwa wa nyota uliochanganyikana na gesi, mavumbi na vitu vingine. Galaxi tunayoishi sisi inaitwa Njia Maziwa "Milky Way".

**NYOTA** ni burungutu kubwa la gesi zinazowaka katika joto kali, zilizoshikiliwa na nguvu ya uvutano (gravity). Nyota yetu ya karibu kabisa inaitwa Jua.

**SAYARI** kama Dunia au Jupita ni tufe kubwa linalozunguka nyota katika njia yake iitwazo obiti. Lakini sayari kwa ujumla haitengenezi mwanga wake yenyewe.

Baadhi ya vitu Vilivyomo Ulimwenguni:







# MAELEKEZO ya JINSI ya KUFURAHIA KITABU HIKI:

1. Kuwa mbunifu kadri uwezavyo.
2. Kuwa mdadisi kadri uwezavyo.
3. Chora na Andika Chochote utakacho!



## TUANZE SASA!

**NENDA NJE.** Unaona nini? Chora picha ya unachokiona!

Angalia nje wakati wa usiku na jaribu kuuchora Mwezi. Je umeweza kuuona?

☐ NDIO!


☐ HAPANA...

Je umeshindwa kuuona mwezi? Kwanini?

Kama umeshindwa kuuona, jaribu tena usiku mwingine mpaka utakapo uona mwezi halafu uuchore.


Our Solar System at size scale:

Paka Rangi Mfumo Wetu wa Jua!



Wanaastronomia wameweza kugundua mamia ya **SAYARI** ambazo hazipo katika mfumo wetu wa Jua. Sayari hizi husafiri kuzunguka nyota nyingine katika galaxi yetu.

Hebu fikiria **SAYARI MPYA** zizungukazo nyota za mbali. Je nyota hizo zina rangi gani? Na ni sayari ngapi zinaizunguka hiyo nyota? Kisha ichore!



Andika shairi kuhusiana na sayari yako uipendayo.

Kichwa/Jina:





Umeivumbua sayari mpya yenye kustaajabisha. Sasa chora picha ya sayari hiyo! Je inaitwaje? Je kuna wanyama na mimea inayoishi kwenye sayari hiyo?


Mchoro wa sayari mpya iliyogunduliwa na mwanasayansi iitwayo: ______________________

______________________ (andika jina la sayari hapa)

CHORA PICHA ZA VIKATUNI ZA SAFARI YAKO YA KWENDA SAYARI YA MERIKI (MARS)!









**MAUMBO SANIFU** / Kundi Nyota (Constellations) ni picha zionekanazo angani wakati wa usiku zinayowakilisha kitu fulani, kama wanyama na binadamu ziliyotengenezwa kwa kuunganisha nyota kwa kutumia mistari ya kufikirika.

Haya ni baadhi ya maumbo sanifu/ Kundi Nyota. Jaribu kuyatazama wakati wa usiku!



Huu ni mchoro wa baadhi ya nyota angani.

Unganisha nukta ili utengeneze umbo **SANIFU / KUNDI** nyota. Unaweza kulipa jina gani?



Ulimwengu Mfukoni Mwako Kitabu cha Mazoezi Kimeandaliwa na:



EU UNIVERSE AWARENESS

Unataka Kujua Zaidi? Tembelea tovuti yetu:

www.eu-unawe.org

Kimetokana na 826 Vitabu vya Mfukoni vya Mazoezi:

www.826national.org

Kimechorwa na Irene Cecile:

www.irenececile.com

Kimetafsiriwa na Mponda Malozo

SEVENTH FRAMEWORK PROGRAMME

